



CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

TAARIFA

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kimeandaa Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika. Kutokana na hivyo, wanajumuiya wote wa Chuo mnaalikwa kuhudhuria kwenye Kongamano hilo.

Kongamano linatarajiwa kufanyika Siku ya Jumatatatu ya tarehe 6/12/2021 saa 2:30 asubuhi katika Ukumbi uliopo Taasisi ya Utalii Kampasi ya Maruhubi. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wanataaluma mahudhurio yenu na wanafunzi wenu ni muhimu ili kulipa hadhi Kongamano hili, ukizingatia kwa Zanzibar SUZA pekee ndiyo iliyopewa dhamana hii kubwa kitaifa ya uandaaji na ufanikishaji wa Kongamano ikiwa ni sehemu ya maadhimisho hayo.

Kauli mbiu: **“Miaka 60 ya Uhuru: Tanzania imara, kazi iendelee”**

**Imetolewa na Ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar**